



DIRISHA LA KUOMBA MIKOPO YA ELIMU YA JUU KUFUNGULIWA RASMI JULAI 15, 2023

HABARI NA MATUKIO

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu HESLB leo Juni 13, 2023 imezindua muongozo na kufungua dirisha la waombaji Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka wa Masomo 2023/2024 .

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga amesema Serikali imetenga Shilingi bilioni 731 zitakazowanufaisha jumla ya wanafunzi 205,000 katika mwaka wa masomo 2023-2024 huku kiasi hicho kikiwa ni ongezeko kutoka Shilingi bilioni 654 za mwaka uliopita wa 2022/2023.

Mara baada ya uzinduzi huo Mhe. Kipanga ameipongeza RITA na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa ushirikiano na kuwezesha mifumo yao ya kidijitali kuzungumza na kubadilishana taarifa zitakazosaidia utoaji wa Mikopo kwa wenye sifa na kwa wakati.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo Abdulrazaq Badru amewataka wanafunzi wenye uhitaji kutembelea na kupata taarifa sahihi kupitia tovuti na mitandao ya kijamii ya Bodi hiyo na ile ya RITA wakati wa uhakiki wa



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga akikata utepe kuzindua muongozo na kufunguliwa kwa dirisha la kupokea maombi ya kutoka kwa wanafunzi wanaoomba Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2023/2024

vyeti vya Kuzaliwa na Vifo mpaka hatua ya mwisho ya kuomba Mkopo wa Elimu ya Juu.

Dirisha la uhakiki litafunguliwa rasmi Julai 15 hadi Oktoba 15, 2023 kwa siku 90 hivyo ni wakati mzuri kwa wanafunzi kutumia fursa ya muda huo kuandaa na kutuma nyaraka sahihi za maombi yao.

Naye Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa RITA Bw. Frank Kanyusi amesema kwa upande wao RITA walianza mapema zoezi la uhakiki wa vyeti vya Kuzaliwa na Vifo Kidijitali kupitia eRITA tangu Juni 01, 2023 na tayari wamepokea maombi ya uhakiki

wa Vyeti vya kuzaliwa 55,549 na Vyeti vya Vifo 3,795 ambayo jumla yake ni 59,344, kati ya hayo, jumla ya maombi ya vyeti vya kuzaliwa na vifo 49,126 sawa na asilimia 82.8 maombi yameshafanyiwa kazi na waombaji kutumiwa majibu yao huku mengine zaidi ya maombi 1,099 yamerejeshwa baada ya kubainika kuwa na mapungufu mbalimbali. Wanafunzi wote watakoomba Mikopo ya elimu ya juu watakiwa kuhakiki vyeti vya Kuzaliwa na Vifo kabla ya kutuma maombi yao Bodi ya Mikopo.



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga akizungumza na Watumishi wa Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhadini- RITA, Wanafunzi wanufaika na Waandishi wa Habari wakati wa uzinduzi wa muongozo wa Waombaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Mwaka wa masomo 2023/2024.



Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa RITA Bw. Frank Kanyusi akiwasilisha maelezo ya hatua iliyofikiwa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhadini RITA katika zoezi la uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa na vifo kwa wanafunzi wanaotarajia kuomba Mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2023/2024..



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Abdul-razaq Badru akitoa neon la utangulizi kati ka hafla ua uzinduzi wa muongozo wa Waombaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Mwaka wa masomo 2023/2024.



Mgeni rasmi Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga akiwa katika picha ya kumbukumbu na viongozi mbalimbali wa Wizara hiyo, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na viongozi wa Wakala wa Usajili Ufulisi na Udhadini RITA mara baada ya hafla ya uzinduzi wa muongozo wa Waombaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Mwaka wa masomo 2023/2024